# FORM 4 END TERM 1 EXAMS KISWAHILI

**Class of KCSE March 2022.**

**For Marking Schemes Call Mr Machuki 0795491185**

**Kenya Educators Contacts: +254795491185**
**kenyaeducators@gmail.com**

**For More e-learning resources contact Kenya educators via the above contacts.**

*JINA..........................................................................USAJILI.........................TAREHE.............*

*SAHIHI......................*

**102/1**
**INSHA**
**KISWAHILI**
**MWISHO WA MUHULA WA KWANZA**
**MUDA: SAA $1^3/_4$**

## MAAGIZO

1. Andika insha mbili: insha ya kwanza ni ya lazima
2. Chagua insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.
3. Kila insha isipungue maneno 400.
4. Kila insha ina alama 20.
5. Zingatia sarufi.
6. Onyesha nambari ya insha unayoandika.

| NAMBARI YA INSHA | ALAMA |
|---|---|
| 1. | |
| 2/3/4 | |

**1.** Andika **tahariri** kuhusu sababu za kudorora kwa usalama katika gatuzi lako.

**2.** Fafanua hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa nchini kukabiliana na umaskini nchini

**3.** Andika insha inayooana na methali ***mchuma janga hula na wa kwao.***

**4.** Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo.

**…niliyagugumia maji hayo kwa pupa na kung'amua kuwa maji ni uhai.**

**JINA**____________________________________________**TAREHE**______________________

**SHULE**________________________________________ **NAMBA YAKO**________________

**SAHIHI**_______________________

**102/2**
**KISWAHILI: KARATASI YA PIL1**
**MWISHO WA MUHULA WA KWANZA**
**MUDA: SAA 2½**

*Hati ya Kuhitimu Mtihani wa Kitaifa wa KCSE*

**102/2**
**KISWAHILI: LUGHA**
**MUDA: SAA 2½**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

a. *Karatasi hii ina kurasa kumi na moja zilizopigwa chapa.*
b. *Andika jina na nambari yako katika nafasi ulioachiwa hapo juu.*
c. *Jibu maswali yote.*
d. *Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
e. *Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

*Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Ilikuwa jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa kusikiliza taarifa ya habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe kiinuamgongo. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi laki mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki.

Watu wengi walinishawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, waziri wa kilimo alitangaza bei mpya. Shilingi 1,500 kwa kila gunia la kilo tisini. Nami nilikuwa naanza kuumakinikia mradi huu.

Baada ya taarifa, nilikoga, nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichukua mara moja. Usingizini niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kulima nilitenga ekari kumi za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wakati wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikati ya mwezi wa Machi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa manyakanga wa kilimo, nililipa shilingi elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejo. Kwanza, nililipa shilingi 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunua magunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilingi 3,300 kila gunia. Mwezi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda. Ili nipate mazo bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilingi 1,000 kila ekari. Mvua ilinyesha vizuri na baada ya siku saba, mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mbegu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua na kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilia kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yananifikia magotini. Hii ikawa ishara kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo 'amonia'.

Gharama yake ikawa shilingi 1,300 kila gunia. Hivyo nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano.

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa mashina. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapitanjia waliajabia mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siku wanaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanisi wangu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno nitakayopata na kukadiria faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa ‘Usikate majani, mnyama hajauawa.’

Bila taarifa wala tahadhari, mvua ilitoweka. Hayakupita majuma mawili mahindi yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahindi, shamba likageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makisio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi ufanyavyo moshi. Lakini ‘Muumba ndiye Muumbua.’ Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha. Muda si muda mahindi yalianza kunawiri. Kumbe tuko lililonivunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwaa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafu huku majani ya mahindi yamechanika kama nyuzi. Niliugua. Baada ya wiki moja, nilipata nafuu. Nilipotazama upande wa shamba niliona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli.

Muda si mrefu mahindi yalirudia hali yake tena, kisha yakakomaa. Harakati za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli hii ikawa shilingi 5,000. Kuvuns, kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500. Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. Habari motomoto siku hiyo ilikuwa. ‘MAHINDI GUNIA 900/=.’ Niligutuka usingizini.

**Maswali**

(a) Andika kichwa mwafaka kwa kifungu hiki cha habari. (alama 1)

(b) Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika? (alama 2)

(c) Taja matatizo matatu yaliyotishia mradi wa msimulizi wa kukuza mahindi (alama 3)

(d) Eleza maana za methali zifuatazo kwa mujibu wa taarifa

(i) Usikate majani, mnyama hajauawa (alama 1)

(ii) Muumba ndiye muumbua (alama 1)

(e) Eleza mambo mawili yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia. (alama 4)

(f) Kwa nini msimulizi alisema maumbile ni kitu cha ajabu? (alama 1)

(g) Eleza maana za;

i. Kinuamgongo (alama 1)

ii. Manyakanga wa kilimo (alama 1)

---

2. **UFUPISHO(ALAMA 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ufupishe kwa mujibu wa maswali uliyopewa
Utafiti umebaini kuwa pana uwiano baina ya lugha inayotumiwa kwa lugha rasmi na kiwango cha umaskini katika nchi, na pia kiwango cha ustawi. Kwa mfano, nchi nyingi za Afrika zimekuwa zikitumia lugha za wakoloni waliozitawala kama lugha rasmi. Nchi hizi zimekuwa zikitumia lugha hizo katika shughuli rasmi, kutoa mafunzo na kupitishia sera muhimu zinazoathiri maisha ya wananchi wote. Kile wasichozingatia ni kuwa, raia wao wengi hawazielewi.

Idadi kubwa ya raia barani Afrika ni wakulima au wasakatonge katika sekta za juakali, uchukuzi na biashara ndogondogo ambao hawana umilisi wa lugha hizo za kigeni. Watu hawa aghalabu huendesha shughuli zao za kila siku kwa kutumia lugha zao za asili, au kama hapa Afrika MAshariki, hutumia Kiswahili ambacho aghalabu hawazingatii usanifu wake. Je, kwa nini tusiokoe na kuauni idadi hii kubwa ya watu ili kuimarisha hali zao kiuchumi, kijamii na ambazo hawazielewi; lugha zinazotumiwa na kufahamika na wachache?

Manufaa ya kutumia lugha inayoeleweka ma kufahamika na wengi kama lugha rasmi ni lukuki yakilinganishwa na maumizi ya lugha za kigeni kama kiingereza, kifaransa, kijerumani au kimandarin. Kwanza, matumizi yake huwawezesha watumiaji kujieleza wakaeleweka vizuri kwa kuwa mkondo wa fikra unatumia lugha wanayoijua, na hivyo wana nafasi ya kuwa wabunifu. Kwa mfano, matumizi ya lugha asili katika utoaji elimu yatahakikisha kuwa wanafunzi wanashiriki kikamilifu katika shughuli zote za kielimu. Hawatakuwa wanafunzi wanaongojea kuelezwa kila kitu bali watajisakuria ili kujizidishia maarifa.
Matumizi ya Kiswahili, lugha inayoeleweka na idadi kubwa ya watu, huhakikisha kuwa ujuzi na maarifa yanayopitishwa si himaya ya kundi dogo tu lililoelimika bali hata wale wasiobahatika kuzielewa lugha hizo za kigeni. Hii ni kwa sababu anayesema kwa lugha ya kigeni husema na ubongo, naye asemaye kwa lugha asili husema na moyo, hivyo basi akaeleweka zaidi katika yale

ayasemayo. Aidha, matumizi haya hutoa nafasi sawa kwa wengi na kuepusha utegemezi wa wakalimani ambao aghalabu hawaeleweki kutokana na kasi ya mazungumzo, au wakatoa fasiri isiyo sahihi. kila mmoja ataweza kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa kutokana na uwezo wa kufasiri sera za serikali na kutoa uamuzi wao wenyewe ikilinganishwa na wakati ambapo sera hizi zinawasilishwa kupitia lugha za kigeni.

Fauka ya haya,matumizi ya lugha inayoeleweka na wengi huwawezesha watu kushiriki na kuchangia katika uimarishaji wa demokrasia kutoka vijijini, hadi kitaifa. Hata hivyo, itashangaza kumwona mzungu akizungumza na wanajamii kwa Kiswahili, naye mwakilishi wa jamii hiyo akiwazungumzia kwa kiingereza. Hii ni njia mmoja ya kuwatenga raia wasioelewa lugha hiyo ya kigeni. Matumizi ya lugha kama hii huhujumu mtagusano baina ya watu. Kwa hivyo, hakisalii tu kuwa lugha rasmi katika katiba bali katika uhalisia.

**Maswali**

(a) Fupisha aya ya kwanza kwa kutumia maneno 35-40 (alama 5)

**Nakala chafu**

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**Nakala safi**

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

(b) Kwa maneno kati ya 100-110, eleza manufaa ya kutumia lugha inayoeleweka na watu wengi kama lugha rasmi katika nchi. (alama 10)

**Nakala chafu**

**Nakala safi**

3. **<u>SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)</u>**

(a) Taja vipasuo viwili vya kaakaa laini. (alama 2)

(b) Andika neno lenye sauti mwambatano. (alama 1)

(c) Weka shadda katika neno lifuatalo ili itoe maana mbili tofauti. (alama 2)

ala

(d) Tumia kiimbo katika sentensi mbili tofauti ili kudhihirisha. (alama 2)

i. Ombi/rai

ii. Amri/kuamuru

(e) Tambulisha vipashio vinne vya sarufi ya Kiswahili. (alama 2)

(f) Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru nafsi ya tatu wingi. (alama 2)

(g) Tumia kivumishi cha pekee katika sentensi kuonyesha umilikaji. (alama 1)

(h) Tumia vihusishi kuonyesha uhusiano wa wakati na kiwango. (alama 2)

(i) Weka maneno haya katika ngeli zake. (alama 2)

i. Miwani

______________________________________________

ii. Wema

______________________________________________

(j) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo. (alama 3)

Hakuwakaribisha

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(k) Bainisha tofauti kati ya mzizi huru na mzizi funge kwa kutoa mifano. ( alama 2)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(l) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika senensi ifuatayo. (alama 2)

Utakapomkabidhi barua hii, nipashe habari

______________________________________________

______________________________________________

(m) Tambua aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Ilitumwa kumlimia nyanya shamba

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(n) Yakinisha sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. (alama 2)

Hakuwasaidia wala hakuwakaribisha kwake.

______________________________________________

______________________________________________

(o) Tambua kirai kihusishi katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Jino la Tamma linauma mara kwa mara.

(p) Tunga sentensi ukitumia neno zawadi kama kitenzi (alama 2)

(q) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Nitamwalika mtondogoo." Fatuma akasema.

(r) Changanua sentensi hii kwa kutumia matawi. (alama 4)

Darasa lilojengwa limefunguliwa leo alasiri.

(s) Kanusha (alama 1)

Sisi ndisi wanafunzi

(t) Tunga sentensi moja ukitumia kiambishi –po- kudhihirisha mahali dhahiri. (alama 1)

**4. <u>ISIMU JAMII (ALAMA 10)</u>**

(a) Eleza maana ya lugha ya taifa. (alama 2)

(b) Eleza sababu tatu zinazofanya watu kubadili na kuchanganya ndimi. (alama 3)

(c) Eleza hatua tano ambazo zimesaidia kukuza lugha ya Kiswahili baada ya uhuru nchini Kenya. (alama 5)

**JINA ______________________________USAJILI __________DARASA _________**

**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasiya3**
**FASIHI**
**MWISHO WA MUHULA WA KWANZA**
**MUDA: SAA 2 ½**

# Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)

## Maagizo

1. *Jibu maswali manne pekee.*
2. *Swali la kwanza ni la lazima.*
3. *Jibu maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizosalia yaani Kigogo, TumboLisiloshiba ,Ushairi na FasihiSimulizi.*
4. *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
5. *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa na kuwa maswali yote yamo.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

| *SWALI* | *UPEO* | *ALAMA* |
|---|---|---|
| *1* | *20* | |
| *2* | *20* | |
| *3* | *20* | |
| *4* | *20* | |
| *5* | *20* | |
| *6* | *20* | |
| *7* | *20* | |

**SEHEMU A: TAMTHILIA**

**P. Kea:** *Kigogo*

1. **Lazima**

*Soma kifungu ufuatao kisha ujibu maswali.*

(a) Utaiondoa karaha,
Usiwe kama juha,
Kujipa bure usheha,
Kutembea kwa madaha,
Eti waenda kwa staha,
Ndani kwa ndani kuhaha,
Domo mbele kama mbweha.
Dume acha mzaha,
Shika lako silaha,
Kujipa mwenyewe raha,
Iwe yako shabaha.

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Taja mtindo huu wa uandishi. (alama 1)

(iii) Bainisha tamathali **moja** ya usemi inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 1)

(iv) Fafanua majukumu ya nafsineni katika tamthilia *Kigogo.* (alama 4)

(b) Kwa kurejelea wahusika mbalimbali katika tamthilia Kigogo. Eleza jinsi mwandishi alivyofanikiwa kutumia nyimbo kuendeleza maudhui, (alama 10)

## SEHEMU B: RIWAYA (CHOZI LA HERI)

**Jibu swali la 2 au 3**

2. “Kumbe hata mja akafanikiwa vipi kielimu na kitaaluma, maisha yake huwa ombwe bila mwana, awe wa kuzaa au wa kulea?”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Taja tamathali moja iliotumika katika dondoo (alama 1)

(c) Onyesha ukweli wa kauli hii ukirejelea wahusika wowote **watano** riwayani (alama 5)

(d) Fafanua umuhimu wa elimu katika jamii ukirejelea riwaya nzima. (alama 10)

3. “Una bahati kupata mfadhili, mimi mzazi wangu wa pekee ni mama ambaye ni muuza samaki na baada ya ule mzozo… biashara imepigwa na mawimbi makali.”

(a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)

(b) Jadili jinsi mwandishi alivyoshughulikia maudhui ya ufadhili. (alama 6)

(c) Ukirejelea hadithi zozote tano riwayani, onyesha jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya hadithi ndani ya hadithi kujenga maudhui.(alama 10)

## SEHEMU C: USHAIRI

**Jibu swali 4 au 5**

4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofauta.

**SIONDOKI**

1.

Eti

Niondoke!

Mimi niondoke hapa

Niondoke hapa kwangu!

Nimesaki; licha ya risasi

Vitisho na mauaji, siondoki.

2.

Mimi

Siondoki

Niondoke hapa kwangu!

Kwa mateke hata na mikuki

Marungu na bunduki, siondoki.

3.

Hapa

Siondoki

Mimi nipahame!

Niondoke hapa kwangu!

Fujo na ghasia zikizuka

Na kani ya waporaji, siondoki.

4.

Haki

Siondoki

Kwangu siondoki

Niondoke hapa kwangu!

Nawaje; waje wanaokuja

Mabepari wadhalimu, siondoki.

5.

Kamwe

Siondoki

Ng’oo hapa kwangu!

Katizame chini mti ule!

Walizikwa babu zangu, siondoki.

6.

Sendi

Nende wapi?

Si'hapa kitovu changu!

Niondoke hapa kwangu

Wangawa na vijikaratasi

Si kwamba hapa si kwangu, siondoki.

7.

Katu

Siondoki

Sihitaji karatasi

Niondoke hapa kwangu

Yangu mimi ni ardhi hii

Wala si makaratasi, siondoki.

MASWALI

(a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)

(b) Fafanua sifa mbili za nafsineni (alama 2)

(c) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)

(d) Eleza umuhimu wa kihisishi katika shairi (alama 2)

(e) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia usambamba katika shairi (alama 2)

(f) Ukirejelea shairi, eleza namna mtunzi alivyotumia idhini zifuatazo (alama 3)

i) Inkisari

ii) Kufinyanga lugha

iii) Udondoshaji wa neno

(g) Taja mbinu tatu za lugha katika shairi (alama 3)

(h) Toa mfano mmoja mmoja wa mishororo ifuatayo (alama 2)

i) mshororo mshata

ii) mshororo kifu

**5. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.**

**SHAIRI LA A**

Falaula ngalijua, singalikuwa kijana,
Kwa sababu sikujua, kajipata mvulala,
Mengi mambo nikajua, nikashinda wasichana,
Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Mwili wangu kabadilli, toto hadi utu uzima,
Sauti yangu kabadili, nikajiola mzima,
Kakiuka maadili, dunia nikaizima,
Kweli ujana moshi, ukienda haurudi.

Masikiongu katonga, herini nikavalia,
Nywele yangu nikasonga, na mikufu kuvalia,
Video pia runinga, tazama bila tulia,
Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Malaika kapata, moyo wangu kapambika,
Jina lake kaloreta, mie wangu malaika,
Penzi langu kalipata,mambo mengi katendeka,
Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.
Moyongu kausumbua, nilipomtia mboni,

Penzi lanisumbua, aingiapo moyoni,

Sautiye kazindua, yatoa nyoka pangoni,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

Penzi lake kalionja, kwangu likawa asali,

Nikawa kionjaonja, kuliwasha kawa kali,

Vitabungu nikakunja, navyo kavitupa mbali,

Kweli ujana ni moshi , ukienda haurudi.

Mzigo kabebesha, ukamwachisha skuli,

Mashakani kaniingisha, nikawa sasa silali,

Kulisaka suluhisho, likawa sasa ghali,

Kweli ujana ni moshi, ukienda haurudi.

**SHAIRI LA B**

Mhariri nipe fursa, nifichue jambo hili,

Nipige wengi msasa, nakusihi tafadhali,

Ukweli wajue sasa, wamakinike ki hali,

Samaki pale barini,kweli huwa si mmoja.

Nawajuza mahawara, pale walipo hakika,
Si ya neni kihasira, ukweli nautamka,
Wayaepuke madhara, wazidi kumakinika
Samaki pale barini, kweli huwa si mmoja.

Dunia imegeuka, waja leo wana shani,
Wazidi kuhangaika, watatizika moyoni,
Utesi umeshazuka, mashambani na mijini,
Samaki pale barini, kweli huwa si mmoja.

Mahaba yakigeuka, hakika huwa ni dhiki,
Ugomvi uje kuzuka, uharibu urafiki,
Wakosane washirika, wapigane kila mwezi,
Samaki pale barini, kweli si mmoja.

Lakini sasa tengeni, vigogo niwasaili,
Iwapo ni hayawani,mpungufu kiakili,
Unisamehe sabini, kwa kosa moja kwa kweli,
Samaki pale barini kweli huwa si mmoja.

Hakika huwa si vyema, kibaya kukimiliki,

Mchongaji nayasema, natangaza uhakika,

Mtu mate huyatema, iwapo hayamezeki,

Samaki pale barini, huwa si mmoja.

Nafumbua fumbo wazi, mnielewe vizuri,

Nafasili ya mapenzi, yalokumbwa nazo zari,

Yalofitinika wazi, hapo ndipo nashauri,

Samaki pale barini, huwa si mmoja.

**Maswali**

a) Jadili maudhui katika shairi A na shairi B (Alama 6)

b) Eleza muundo wa shairi la A (Alama 4)

c) Toa mifano ya uhuru wa utunzi uliotumiwa katika shairi la B. (Alama 2)

d) Andika ubeti wa nne wa shairi la A katika lugha nathari. (Alama 4)

e) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika mashairi haya. (Alama 4)

i) Nikajiola

ii) Mzigo kambebesha

iii)Shani

iv) Zari

## SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI

***6.*** *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

**(a)** **A**: Kumbe mambo yenyewe rahisi hivi?

**B**: Rahisi, lakini usije ukababakwa tena

**A**: Hapana, safari hii itakuwa zamu yako. *(Alimrudishia … huku akichekacheka)*

**C**: Hapajaharibika mambo mama'ngu. Kwani la ajabu lipi? Sasa miye namsubiri Bakari mpya tu, hichi kikongwe nikipe talaka.*(Akitabasamu)*

**D**: Haachwi mtu hapa. Tutabanana humo humo. Yeye atakuwa mke mdogo na mimi mkubwa.

(i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 1)

(ii) Toa sababu **mbili** kuthibitisha jibu lako la (i) hapo juu. (alama 2)

(iii) Eleza manufaa saba ambayo jamii hunufaika nayo kwa kushiriki katika kipera hiki. (alama 7)

**(b)** *Soma kifungu ufuatao kisha ujibu maswali*.

Siwezi kuhutubu. Mimi sikuwafundisha ubaguzi. Kwa nini mnabaguana? Kwa nini hamukuwapa watu wa matabaka yote nafasi ya kuzungumza? Kwa nini? Kwa nini mnafanya hali hii ya kuwa kuna watu na nusu watu? Nataka wazungumze wale ambao hawata sifu tu.

(i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 2)

(ii) Eleza mitindo mitatu katika kifungu hiki. (alama 3)

(iii) Eleza majukumu matano ya kipera hiki katika jamii. (alama 5)

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda**: Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine

*"Tulipokutana Tena"* **(Alifa Chokocho)**

5 (a) Halikuwa jambo la kawaida maana maji yalikuwa hayapatikani karibu pale kijijini petu. Sharti mtu aende masafa marefu kuyatafuta. Na sabuni? Sabuni ilikuwa kitu cha anasa kwa familia yetu. Wazazi wangu hakuwa na uwezo wa kununua Sabuni. Labda mara moja moja siku za sikukuu.

(i) Eleza muktatha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Eleza majukumu mawili ya **takriri** katika dondoo hili. (alama2)

(iii) Kwa kurejelea hadithi*Tulipokutana Tena* jadili jinsi haki za watoto zinavyokiukwa.(alama 6)

(b) Jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa ukirejelea hadithi zifuatazo: (alama 10)

(i) Masharti ya Kisasa

(ii) Ndoto ya Mashaka